

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI GEITA

MKOA WA GEITA

Simu No. 0282520437  
Nukuhi No. 0282520437  
Barua Pepe: [td@geitatc.go.tz](mailto:td@geitatc.go.tz).  
Tovuti : [www.geitatc.go.tz](http://www.geitatc.go.tz)



Halmashauri ya Mji,  
S.L.P 384,  
GEITA.

TAREHE: 14/07/2020

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA DEREVA WA MITAMBO DARAJA II  
(EXCAVATOR) - NAFASI 1- LINARUDIWA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita anawatangazia nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa za kujaza nafasi ya uendeshaji wa mtambo wa "Excavator" kama ilivyoorodheshwa katika tangazo hili;-

**1.0 MAJUKUMU YA KAZI**

- Kuendesha mitambo chini ya usimamizi wa dereva mitambo mwenye uzoefu.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa.

**2.0 SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- Kuajiriwa mwenye leseni ya daraja G ya uendeshaji Mitambo.

**NB:** Wenye leseni zenye sifa za ziada kama daraja F, E na C1 watapewa kipaumbele.

**3.0 MASHARTI YA JUMLA**


- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (Detailed CV) yenye anuani ya Posta na namba ya simu ya kuaminika ikiambatana na majina ya wadhamini watatu (3).
- Maombi yaambatanishwe na nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo ya uendeshaji wa mitambo na vyeti vya kidato cha Nne vilivyodhibitishwa na Mwanasheria.
- Muombaji aambatanishe picha ndogo ya rangi (passport size) ya hivi karibuni.
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form VI and form IV result slips) HAVITAKUBALIWA.
- Waombaji waliosoma elimu ya kidato cha nne (4) nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA).
- Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma wapitishwe barua zao za maombi ya kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

**4.0 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya mshahara TGOS A kwa mwezi.

**5.0 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **28/07/2020** saa **9:30** alasiri. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwenda kwa Mkurugenzi, Halmashauri ya Mji, **S.L.P 384 GEITA**. Waombaji watakaokidhi vigezo watajulishwa kwa njia ya simu na matangazo ili kuweza kuja kwenye usaili.

  
Eng. Modest J. Apolinary,  
MKURUGENZI,  
HALMASHAURI YA MJI,  
GEITA.  
MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MJI  
GEITA.